TANGAZO LA SERIKALI NAMBA 25 LA TAREHE 10/03/2006
SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA 1982
NAMBA 9 YA MWAKA 1982.

(Zimetungwa chini ya Vifungu vya) 6 na 13 (1)

SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI (ADA NA USHURU) ZA MWAKA 2006

Jina na tarehe ya kuanza kutumika:

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Moshi (Ada na Ushuru) za mwaka 2006, na zitaanza kutumika kuanzia tarehe zitakapochapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la Kutumika:

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.

Tafsiri:

3. Katika Sheria Ndogo hizi:

"Ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa ajili ya huduma, vibali na Leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi;

"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Moshi;

"Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, pamoja na afisa yeyote yule ambaye atakuwa anatekeleza shughuli za Mkurugenzi;

"**Afisa muidhiniwa**" Maana yake ni mtu yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kutekeleza jambo lolote chini ya Sheria hizi Ndogo;

"Kibali cha ujenzi" maana yake ni kibali cha ujenzi kinachotolewa na Halmashauri chini ya kanuni za Mijini sura Namba 101 au chini ya Sheria hizi Ndogo au Kanuni zilizofanyia mabadiliko kanuni hizo;

"Maeneo ya Kati" maana yake maeneo yaliyopo katikati ya Mji yaani Central Business District (CBD);

"**Maeneo mengine"** Ni maeneo yote katika Manispaa ambayo si maeneo ya kati na;

"Waziri" Maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

Ada na Ushuru:

4. (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru ulioorodheshwa kwenye Jedwali la Sheria hizi Ndogo kwa huduma, vibali na Leseni zitolewazo na Halmashauri.

(2) Ada na Ushuru utozwao chini ya sheria hizi Ndogo unapaswa kulipwa kabla ya mlipaji kupata huduma au leseni au kibali husika na kwa vyovyote vile haitazidi tarehe 30 ya mwezi wa Juni ya mwaka unaolipwa.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kubadilisha viwango vya Ada na Ushuru muda wowote kadri itakavyoona kuwa inafaa kufanya hivyo.

(4) Hata hivyo viwango hivyo vitakuwa ni halali iwapo kusudio la kuvibalidilisha litatolewa taarifa na kubandikwa kwenye mbao za matangazo siku kumi na nne kabla ya kuanza kutumika.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru:

5. Utakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa ada na ushuru utozwao kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kulipa ushuru na au ada kama zilivyoelekezwa kwenye jedwali.

Ada na ushuru kulipwa Halmashauri:

6. (1) Ada na Ushuru utozwao kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo cha kukubali malipo hayo.

(2) Hautakuwa ni utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, mtu yeyote kudai kuwa amelipa ada na ushuru lakini hakupewa stakabadhi.

Madaraka ya Mkurugenzi

7. Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na madaraka ya kufifisha kosa kwa kumtaka mtu aliyekiri kufanya kosa chini ya Sheria hizi Ndogo kulipa kiasi cha fedha kisichozidi kiwango cha juu cha faini kilichowekwa chini ya Sheria hizi Ndogo.

Ilani

8. (1) Mtu yeyote ambaye atashindwa kutekeleza maagizo yoyote yatakayotolewa kwa Ilani na Halmashauri chini ya Sheria hizi Ndogo atakuwa ametenda kosa.
(2)Bila kujali masharti yaliyomo kwenye kifungu kidogo cha (1) cha Sheria hizi Ndogo itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kutotii Ilani iliyotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria hizi Ndogo.

Makosa na adhabu

9. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Sheria hizi Ndogo atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kinachozidi miezi 12 au vyote, Kifungo na faini kwa pamoja.

Kufutwa Sheria Tangazo la Serikali Na. 439/1996

10. Sheria Ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Moshi (Ada na Ushuru) za mwaka 1996 zinafutwa

JEDWALI

1. ADA YA KUKODI VIWANJA NA MITAMBO/VIFAA VYA HALMASHAURI

(i)	Nyumba za kuishi (ambayo siyo ya watumishi)	(i) Kulingana na Mkataba		
(ii)	Nyumba ya biashara	(ii)Kulingana na Mkataba		
(iii)	Kumbi za Halmashauri-Ukumbi mkubwa		Shs.50,000/=	Kwa siku
		Ukumbi mdogo	Shs, 30,000/=	Kwa siku
(iv)	Viti vya Halmashauri	(i)Vikubwa	Shs.200/=	Kwa siku
		(ii) Vidogo	Shs.100/=	Kwa siku
(v)	Uwanja wa Mashujaa		Shs.50,000/=	Kwa siku
(vi)	Lori		Shs.80,000/=	Kwa siku

(vii)	Tingatinga	Shs.70,000/=	Kwa saa
(viii)	Mitambo mingine	Shs.35,000/=	Kwa saa

2. ADA YA KUPIMA WAHUDUMU

(1) Kila Mhudumu wa nyumba ya kulala wageni, Hoteli, Mgahawa, Muuzaji wa vyakula vilivyopikwa Au Kukaangwa anawajibika kujisajili kwa Halmashauri ili kubainisha ukamilifu wa afya yake kuendesha shughuli hiyo kwa mujibu wa Kifungu Namba 32, 33, 34, 39,43, 44, 51 na 52 vya Kanuni za Miji, Sura namba 101……...Shs 5,000/= kwa kila miezi sita

3. ADA YA KUPULIZIA DAWA

(i) Ada ya kupulizia dawa ya wadudu(Fumigation) ambayo itafanywa na Halamashauri Shs. 5,000/= kwa mita za miraba za eneo(Per square Meter) .

(ii) Ada ya usimamizi wa kunyunyiza dawa ya wadudu unaofanywa na watu binafsi Shs, 2000/= kwa kazi.

4. **ADA ZA HUDUMA ZA GARI LA WAGONJWA NA HUDUMA ZA MAZISHI**.

(i) Ada za huduma za gari la wagonjwa Shs. 1000/= kwa safari
(ii) Huduma za mazishi. Shs 2000/=

5. ADA YA UKAGUZI

(i) Hoteli…….Shs.10,000/= kwa Mwaka
(ii) Mgahawa/Baa…… ……...Shs.20,000/= kwa Mwaka
(iii) Nyumba za kulala wageni…….Shs.20,000/= kwa Mwaka
(iv) Viwanda…….Shs.30,000/= kwa Mwaka
(v) Biashara nyinginezo……..Shs.10,000/= kwa Mwaka
(vi) Ukaguzi wa dharura……...Shs.20,000/= kwa Mwaka

6. ADA YA UZOAJI TAKA

(i) Hotel …….. …….Shs.180,000/= kwa Mwaka
(ii) Mgahawa……..Shs. 60,000/= kwa Mwaka
(iii) Duka la Jumla ……**.....**Shs. 60,000/= kwa Mwaka
(iv) Viwanda vikubwa/Taasisi……Shs.780,000/= kwa Mwaka
(v) Viwanda Vidogo……Shs.260,000/= kwa Mwaka
(vii) Biashara nyinginezo…….Shs. 36,000/= kwa Mwaka
(viii) Nyumba za kuishi…….Shs. 12,000/= kwa Mwaka
(ix) Masoko/ Bus stend……...Shs. 15,000/= kwa Tripu
(x) Ada ya Ushuru wa Dampo……...Shs. 5,000/= kwa Tripu
(vi) Ada ya kupiga / kunyunyiza dawa……...Shs. 5,000/= kwa Chumba

7. ADA YA UNYONYAJI MAJI MACHAFU KATIKA VYOO KWA KUTUMIA MAGARI YA HALMASHAURI

(i)	Maeneo ya Biashara	(i) Shilingi 25,000/= kwa kila safari moja
(ii)	Maeneo ya Makazi	(ii)Shilingi 15,000/= kwa kila safari moja
(iii)	Nje ya Eneo la Halmashauri	(iii)Shilingi 30,000/=kwa kila safari moja
		Na nyongeza ya Tshs 500/= kwa kila kilometa

8. **ADA YA MABADILIKO YA MATUMIZI YA ARDHI KAMA IFUATAVYO**;-

(i) Makazi kuwa Biashara…….....Tshs.20,000/=
(ii) Makazi kuwa Viwanda……Tshs.25,000/=
(iii) Biashara kuwa Viwanda…… ……Tshs.25,000/=
(iv) Makazi kuwa Biashara n.k
Kuwa Housing estate……Tshs.20,000/=
(v) Makazi kuwa Biashara n.k.
Kuwa Block of flats …….Tshs.20,000/=
(vi) Viwanda Biashara n.k
Kuwa Kituo cha Mafuta……Tshs.30,000/=
(vii) Kugawanya Kiwanja au Shamba……..Tshs.25,000/=
(viii) Kuhakiki Miliki……Tshs.5,000/=kwa kiwanja

9. ADA ZA MAEGESHO NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

	Aina ya magari	**Kiwango cha Ada**
(i)	Taxi	Sh. 60,000/= kwa mwaka
(ii)	Mabasi madogo abiria 25-30	Sh.1,000/= kwa safari
(iii)	Mabasi makubwa	Sh.1,000/= kwa safari
(iv)	Mabasi ya mzunguko Mjini	Sh.240,000/=kwa mwaka
(v)	Lor Tani 2-5	Sh.180,000/=kwa mwaka
(vi)	Pick Up	Sh.60,000/= kwa mwaka
(vii)	Magari yasiyokuwa ya biashara Yanayoegeshwa katika eneo la Mji	Sh. 200/= kwa saa
(viii)	Kibali maalumu cha kuegesha	Sh.30,000/= kwa mwaka
(ix)	Kibali maalumu cha kuhodhi maegesho	Sh. 50,000/= kwa mwaka
(x)	Ada ya usajili wa magari ya biashara	Sh. 10,000/= kwa safari

10. ADA YA KUZINGIRA NA KUWEKA MAJUKWAA KATIKA MAENEO YA KATI NA MAENEO MENGINEYO KUTEGEMEA NA UKUBWA

	MAENEO YA KATI	**MAENEO MENGINEYO**	**MUDA**
(i)	500/= kwa futi	300/= kwa futi	Chini ya wiki 2
(ii)	1,500/=kwa futi	1,000/= kwa futi	Kati ya wiki 2 na 4
(iii)	2,000/=kwa futi	1,500/=kwa futi	Kati ya wiki 4 na 9
(iv)	2,500/= kwa futi	2,000/=kwa futi	Kati ya wiki 9 na 12
(v)	4,000/= kwa futi	3,500/=kwa futi	Kati ya wiki 12 na 52
(vi)	5,000/= kwa futi	4,500/= kwa futi	Zaidi ya mwaka

11. USHURU WA MASOKO NA MAGULIO

NA.	**ZAO**	**USHURU**
1.	Tenga 10 Nyanya	400/=
2.	Tenga la Samaki	400/=
3.	Gunia la Mahindi	400/=
4.	Gunia la Mihogo,Viazi vitamu,Machungwa,Nazi n.k	400/=
5.	Gunia la Mchele/ Ngano	600/=

6.	Gunia la Mpunga	400/=
7.	Gunia la Vitunguu aina zote	700/=
8.	Mkungu wa ndizi mbivu	200/=
9.	Gunia la karoti	500/=
10.	Mkungu wa ndizi mbichi	200/=
11.	Debe la ndizi mbivu	200=
12.	Gunia la Maharage Dengu, Kunde	600/=
13.	Ushuru wa mboga matunda (Kwa siku) masoko ya	200/=
14.	Mbuyuni, Kiusa, Soko Kuu na Kiborloni	150/=
15.	Box ndogo	300/=
16.	Box kubwa	400/=

12. ADA YA KIBALI CHA UJENZI

Maombi mapya Tshs 25,000/=
Kuomba upya baada ya maombi mapya kuisha Tshs 15,000/=

13. ADA YA MAEGESHO YA MAGARI

(a) Maegesho maalumu kwa ajili ya kuegesha magari Tshs 30,000/= kwa mwezi
(b) Maegesho ya Umma Tshs 200/= kwa gari-kwa **saa**

14. **ADA YA MATANGAZO YA BIASHARA YALIYOSIMIKWA, KUCHORWA KUCHAPISHWA NA KUBANDIKWA KATIKA ENEO LOLOTE LA HALMASHAURI.**

(i) Maombi ya kufanya matangazo Tshs. 3,000/=
(ii) Yaliyowekwa taa (non-iluminated)-shilingi 500/= kwa kila sentimeta mia moja za eneo kwa mwaka
(iii) Lenye mwanga (illuminated Advertisement) shilingi 1,500/= kwa kila sentimeta mia moja za eneo kwa mwaka
(iv) Mengineyo Tshs 500/= -kwa kila Sentimeta mia moja za Eneo.

15. ADA YA HUDUMA ZA MACHINJIO NA UKAGUZI

(i) Ada ya Uchinjaji/Machinjio Shilingi 2,000/= kwa kila Ng'ombe
Shilingi 1,000/= kwa kila Nguruwe
Shilingi 600/= kwa kila Mbuzi/Kondoo

(ii) Ada ya ukaguzi Shilingi 500/= kwa kila Ng'ombe
Shilingi 500/= kwa kila Nguruwe
Shilingi 400/= kwa kila Mbuzi/Kondoo
Shilingi 50/= kwa kila Kuku

16. ADA YA KIBALI CHA KUCHIMBA/ KUKATA BARABARA

(i) Barabara ya lami- Shs. 25,000/= kwa mita moja za mraba (per sq. meter).
(ii) Barabara ya udongo Shs. 20,000/= kwa mita

Mhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi umewekwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 28 Mwezi waApril 2005 na kubandikwa mbele ya:-

L.S.TARIMO
MSTAHIKI MEYA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

JOEL. M. SHIMBA
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

NAKUBALI
7 Oktoba, 2005
DODOMA
MHE BRIG. JEN. MSTAAFU H.A.H.NGWILIZI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TANGAZO LA SERIKALI NAMBA 139 LA TAREHE 27/4/2012
SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)
SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6 (1) na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI ZA MWAKA, 2011

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1 Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushauru) (Marekebisho) za Halmashauri ya Manispaa ya Moshi za mwaka 2011, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Moshi za mwaka 2006 ambazo zitaitwa Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Eneo la kutumika

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika kwenye eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.

Marekebisho katika kifungu cha Tafsiri

3 Kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo kuu kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya neno

"Boda Boda" baada ya tafsiri ya neno "Ada" kama ifuatavyo:-,

"Boda Boda" maana yake ni Pikipiki zitumiazo magurudumu mawili (motocycle) zenye uwezo wa kubeba abiria mmoja na dereva pamoja na Pikipiki zinazotumia magurudumu matatu (tricycle) maarufu kama Bajaji zenye uwezo wa kubeba abiria watatu pamoja na dereva"

Marekebisho ya kufungu cha 9 cha Sheria Ndogo Kuu.

4 Kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo Kuu kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa.

"Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu kumi (10,000/=) na isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo."

JEDWALI

1. Kifungu cha kwanza (1) cha Sheria Ndogo Kuu katika Jedwali kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa:-

   ADA YA KUKODI VIWANJA NA MITAMBO NA VIFAA VYA HALMASHAURI

   (i) Nyumba za kuishi (ambazo siyo za Watumishi) kulingana na Mkataba .
   (ii) Nyumba ya biashara –Kulingana na Mkataba
   (iii) Kukodisha Ukumbi wa Halmashauri 200,000/= kwa siku
   (iv) Kukodisha viwanja vya Halmashauri (Mashujaa na Majengo) 300,000/= kwa siku
   (v) Kukodisha viti vya Halmashauri
      (i) Kidogo 500/= kwa siku
      (i) Kikubwa 1,000/= kwa siku
   (vi) Kukodisha Lori 100,000/= kwa safari
   (vii) Tingatinga siyo chini ya 100,000/= kwa saa
   (viii) Mitambo Mingine 50,000/= kwa siku

2. Kifungu cha tatu (3) cha Sheria Ndogo kuu katika Jedwali kinafutwa na

badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa:-

ADA YA KUPULIZA DAWA YA WADUDU

(i) Ada ya kupuliza dawa ya wadudu (Furmagation) ambayo itafanywa na Halamashauri 10, 000/= kwa mita za Mraba

(ii) Ada ya usimamizi wa kunyunyizia dawa ya wadudu inayofanywa na watu binafsi 50,000/= kwa kazi

3. Kifungu cha tano (5) cha Sheria Ndogo Kuu katika Jedwali kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa:-

ADA YA UKAGUZI

(i)	Ada ya Ukaguzi wa Hoteli	Shs.30,000/= kwa Mwaka
(ii)	Mgahawa/Baa	Shs.20,000/= kwa Mwaka
(iii)	Nyumba za kulala wageni	Shs.20,000/= kwa Mwaka
(iv)	Viwanda	Shs.50,000/= kwa Mwaka
(v)	Biashara nyinginezo	Shs.10,000/= kwa Mwaka
(vi)	Ukaguzi wa dharura	Shs.20,000/= kwa Mwaka

4. Kifungu cha (6) cha Sheria Ndogo kuu katika Jedwali kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa.

ADA YA UZOAJI TAKA

(i)	Hotel	Shs.260,000/= kwa Mwaka
(ii)	Mgahawa	Shs. 80,000/= kwa Mwaka
(iii)	Shopping Molls	Shs 500,000/= kwa mwaka
(iv)	Duka la Jumla	Shs. 60,000/= kwa Mwaka
(v)	Viwanda vikubwa/Taasisi	Shs.780,000/= kwa Mwaka
(vi)	Viwanda Vidogo	Shs.260,000/= kwa Mwaka
(xi)	Biashara nyinginezo	Shs. 36,000/= kwa Mwaka
(xii)	Nyumba za kuishi	Shs. 12,000/= kwa Mwaka
(xiii)	Masoko/ Bus stend	Shs. 15,000/= kwa Safari
(xiv)	Ada ya Ushuru wa Dampo	Shs. 5,000/= kwa Safari
(vii)	Ada ya kupiga / kunyunyiza dawa`.	Shs. 5,000/= kwa Chumba

5. Kifungu cha (7) cha Sheria Ndogo kuu katika Jedwali kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa.

ADA YA UNYONYAJI MAJI MACHAFU KATIKA VYOO KWA KUTUMIA MAGARI YA HALMASHAURI

(i)	Maeneo ya Biashara	40,000/= kwa kila safari moja
(ii)	Maeneo ya Makazi	40,000/= kwa kila safari moja
(iii)	Nje ya Eneo la Halmashauri	40,000/=Kwa kila safari moja
	Na nyongeza ya shilingii	1,000/= kwa kila kilometa
	inayozidi mara baada ya kutoka nje ya Halmashauri	

6. Kifungu cha kumi (10) cha Sheria Ndogo kuu katika Jedwali kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa:-

ADA YA KUZINGIRA NA KUWEKA MAJUKWAA KATIKA MAENEO YA KATI NA MAENEO MENGINEYO KUTEGEMEA NA UKUBWA

	MAENEO YA KATI	**MAENEO MENGINEYO**	**MUDA**
(i)	1,000/- kwa futi-2	600 kwa futi	Chini ya wiki
(ii)	3,000/=kwa futi-	2,000/= kwa futi	Kati ya wiki 2 na 4
(iii)	4,000/=kwa futi	3,000/=`kwa futi	Kati ya wiki 4 na 9
(iv)	5,000/- kwa futi	4,000/=-kwa futi	Kati ya wiki 9 na12
(v)	8,000/= kwa futi 52	7,000/= kwa futi	Kati ya wiki 12 na
(vi)	10,000/=kwa futi	9,000/= kwa futi	Zaidi ya mwaka

7. Kifungu cha kumi na mbili (12) cha Sheria Ndogo kuu katika Jedwali kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa:-

ADA YA KIBALI CHA UJENZI

(i) Maombi mapya

Makazi	Tshs 40,000/=
Biashara/ghorofa	Tshs 40,000/= biashara/kila ghorofa
Viwanda	Tshs 400/= kwa kila mita 1 ya mraba ya eneo la ujenzi
Taasisi	Tshs 300/=kwa kila mita 1 ya mraba ya eneo la ujenzi
Vituo vya Mafuta	Tshs 200,000/=

(ii) Maombi baada ya muda wa kibali kuisha

Makazi	Tshs 25,000/=
Biashara/ghorofa	Tshs 50,000/= biashara/kila ghorofa
Viwanda	Tshs 100,000/=
Taasisi	Tshs 75,000/=
Vituo vya Mafuta	Tshs 50,000/=

(iii) Kibali cha ujenzi minara ya simu Tshs 500,000/=

8. Kifungu cha kumi na nne (14) cha Sheria Ndogo kuu katika Jedwali kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa;-

USHURU WA MATANGAZO YA BIASHARA YALIYOSIMIKWA, KUCHORWA, KUCHAPISHWA NA KUBANDIKWA KATIKA ENEO LOLOTE LA HALMASHAURI

(i) Maombi ya kufanya matangazo…….Tshs. 3,000/=

(ii) Matangazo yasiyowaka taa (non illuminated)…….....Tshs 1,000/= kwa kila sentimita mia moja za eneo kwa mwaka

(iii) Matangazo yenye mwanga (illuminated)……Tshs 3,000/= kwa kila sentimita mia moja za eneo kwa mwaka

(iv) Matangazo yanayomeremeta (Unmated)……..Tshs 4,000/= kwa kila sentimita mia moja za eneo kwa mwaka

(v) Matangazo mengineyo ……Tshs 500/= kwa kila sentimita mia moja za eneo kwa mwaka

9. Kifungu cha kumi na tano (15) cha Sheria Ndogo kuu katika Jedwali kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa;-

USHURU WA MACHINGJIO NA UKAGUZI WA NYAMA

(i)	Ushuru wa Machinjio Ng'ombe	Shilingi 5,000/= kwa kila
		Shilingi 2,000/= kwa kila Nguruwe
	Mbuzi/Kondoo	Shilingi 1,000/= kwa kila
(ii)	Ada ya ukaguzi	Shilingi 500/= kwa kila Ng'ombe
		Shilingi 500/= kwa kila Nguruwe
	Mbuzi/Kondoo	Shilingi 400/= kwa kila
		Shilingi 50/= kwa kila Kuku

10. Kifungu cha kumi na sita (16) cha Sheria Ndogo kuu katika Jedwali kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa;-

ADA YA KIBALI CHA KUCHIMBA/ KUKATA BARABARA

(i) Barabara ya lami Tshs 50,000/= kwa mita moja za mraba (per sq meter).

(ii) Barabara ya udongo Tshs.40,000/= kwa mita moja za mraba (per sq meter).

11. Kifungu cha kumi na saba (17) cha Sheria Ndogo kuu katika Jedwali kinafutwa na badala yake kifungu kifuatacho kinawekwa;-

ADA YA MATUMIZI YA UWANJA (GROUND RENT) NDANI YA ENEO LA HALMASHAURI KWA SHUGHULI ZA BIASHARA

i. Ada ya kuendesha biashara viosks kuzunguka Soko la Kati, Soko la Kiusa, Mbuyuni na Kituo Kikuu cha Mabasi Tshs. 180,000/= kwa mwaka.

ii. Ada ya kuendesha sehemu za kutengenezea magari nguvu kazi garages katika viwanja karibu na machinjio ya Bomambuzi Tshs, 180,000/= kwa mwaka

iii. Ada ya kuendesha biashara na viosks nguvu kazi garages Uwanja wa Jamhuri na Mtaa wa Dar es Salaam Tshs. 90,000/= kwa mwaka

iv. Ada ya kuendesha biashara ya viosks na nguvu kazi Soko na Uwanja wa Majengo Tshs, 60,000/= kwa mwaka

v. Ada ya kuendesha biashara ya viosks na nguzu kazi garages katika masoko ya Ngangamfumuni, Kiborloni, Pasua, Bomambuzi na maeneo mengine yoyote ambayo hayajatatwa Tshs.30,000/= kwa mwaka

Mhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililotolewa kwenye kikao cha Mkutano wa Halmashauri kilichofanyika tarehe 28/09/2011 na kushuhudiwa na:-

BERNADETTE KINABO
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

JAPHARY MICHAEL
MSTAHIKI MEYA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

NAKUBALI

MHE. MIZENGO P. PINDA (MB)
WAZIRI MKUU